KUELEKEA MABADILIKO 2010 ADAYE...

Cheche za Fikra

JUZUU 13 TOLEO 46

AUGUSTI 27, 2010

KIJARIDA CHA BURE— CHAPA NAKALA 2 NA GAWA BURE!

MTANANGE WA DEMOKRASIA 2010

AFYA YA KIKWETE BADO YATATIZA!



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Na. Mwandishi Wetu

Kuanguka kwa mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bw. Jakaya Kikwete mbele ya maelfu ya wanachama, mashabiki na wananchi siku ya Jumamosi iliyopita kwenye viwanja vya jangwani kumeacha maswali na gumzo kubwa juu ya afya ya mgombea huyo na hekima ya kuendelea na kampeni yake.

Tukio hilo ambalo lilikuja dakika chache tu baada ya Mwenyekiti huyo wa CCM Taifa kuanza kuhutubia na kuelezea mafanikio ya
(Inaendelea Uk. 2)



Rais Kikwete muda mfupi kabla ya kuanguka Jangwani

Kijarida Ulichoshika

- Kinatoka kila wiki
- Ni cha bure kabisa!
- Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!
- Ndiyo chanzo huru zaidi cha habari na maoni.
- Ni kijarida chako!
- Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa; kiri chanzo!

Ndani ya Toleo Hili

Afya Tete ya Kikwete	1,2, 3
Tukutane Jangwani	1,4
CUF nao vipi?	3
Jessy: Kurushana moyo?	4
Hasira ya Baba—2	5
Maoni ya Mhariri	5
Picha, Katuni na Maoni	6

TUKUTANE JANGWANI J'MOSI—DR. SLAA

Na. Freddy Katunzi

Mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo Dr. Willibrod Slaa ametoa wito kwa maelfu ya wakazi wa jiji la Dar na maeneo ya jirani kukutana nao Jangwani siku ya Jumamosi ambapo anatarajiwa kutoa hotuba ambayo ameitaja kuwa ni ya "kihistoria" akizindua kampeni yake ya Urais na kampeni za wagombea Ubunge na Udiwani nchini kupitia Chadema.

Dr. Slaa ambaye amechelewesha kuanza kampeni yake kwa ajili ya kupata muda wa kupumzika na kupona kufuatia upasuaji wa mkono wake amedokeza kuwa kampeni ya itatoa maono mapya kabisa ya kiuongozi na utawala kwa taifa yakiwa ni tofauti kabisa na yale ambayo yameonekana kushindwa kwa miaka 50 iliyopita chini ya utawala wa CCM.
(Inaendelea Uk. 4)

uongozi wake katika miaka mitano uliyopita lilisababisha hofu kubwa iliyotanda katika viwanja hivyo na kwa mamilioni ya Watanzania waliokuwa wakifuatilia tukio hilo moja kwa moja kwa njia ya luninga.

Akielezea mafanikio yake na ahadi yake dhidi ya kupambana zaidi na rushwa Rais Kikwete alisema "Tunawaahidi Watanzania, wakitupa ridhaa yao, tutafanya zaidi; tutatekeleza mengi na tutafanya mengi zaidi; aisee, tupeni ridhaa yenu tutafanya mengi zaidi tuta(akauma maneno)". Baada ya maneno hayo alishindwa kuendelea kusimama na akaanguka nyuma ambapo alidakwa na wasaidizi wake ambapo kundi la maafisa wa usalama lilifanya hima kumnyanyua na kumbeba kumpeleka kwenye gari la huduma ya afya lililokuwa pembeni tu ya jukwaa hilo.

Habari za kuanguka kwa Kikwete jukwaani zilianza kusambaa kama uvumi wa habari mbaya kwa kutumia mitandao ya simu na ya intaneti huku wananchi sala na dua zikitolewa na watu kuombea kuwa tukio hilo lisingeishia kubaya. Pamoja na mshtuko huo baada ya muda mfupi Rais Kikwete alionekana kurejea katika afya yake na kurudi jukwaani ambapo alishindwa kuendelea na hotuba ndefu aliyoipanga na hatimaye kufungua kampeni hiyo kwa maneno mafupi na hatimaye kuondoka uwanjani hapo.

Tukio hilo lilisababisha na limeendelea kusababisha minong'ono kati ya wananchi juu ya afya ya Rais Kikwete hasa kwa sababu inakumbukwa kuwa hili si tukio la kwanza la Rais Kikwete kuishiwa na nguvu jukwaani na kuanguka hadharani. Wananchi wengi wanakumbuka matukio mengine mawili ambapo Rais Kikwete alianguka hadharani la kwanza likiwa ni wakati wa kufunga kampeni ya Urais ya 2005 kwenye viwanja hivyo hivyo vya Jangwani ambapo maelezo yaliyotolewa wakati ule ndio yametolewa tena kuwa "ilitokana na swaumu". Lakini vile vile miaka michache tu iliyopita Rais Kikwete alianguka tena huko Mwanza akiwa katika jumuiya ya kanisa la AIC ambapo ilisababisha madaktari wake kulazimika kutoa historia ndefu ya afya ya Rais Kikwete na kudokeza juu ya matatizo ambayo bila ya shaka bado yanamsumbua hadi hivi sasa.

Vile vile zipo taarifa katika duru la intelligentsia kuwa hali hii ya kuanguka haiishi katika hadhara tu bali matukio kama haya yamewahi kushuhudiwa ndani ya Ikulu na kwenye misafara yake nje ya nchi. Na yote hayo yanashindwa kuelezewa kuwa ni kutokana na "kufunga". Hata hivyo maelezo ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara kuelezea hali hiyo ni upungufu wa sukari mwilini ambao unamsababishia Kikwete kupoteza nguvu katika hali ambayo kitaalamu inaitwa ni hypoglycemia (haipoglasimia). Hata hivyo tetesi nyingine zisizothibitishwa zinadokeza kuwa yawezekana ana kifafa kidogo (petit mal epilepsy) ambayo husababisha kupoteza fahamu kwa sekunde chache.

..Taarifa ya Dr. Mfisi ya mwaka jana ipo kwa Mwanakijijji.Com ..

Kufuatia tukio la kuanguka Rais kule Mwanza Oktoba 4, 2009 wakati wa kuadhimisha sherehe za miaka 100 ya Kanisa la African Inland (AIC) kwenye Uwanja wa Kirumba madaktari wake walilazimika kutoa taarifa ndefu juu ya afya ya Rais. Akiandika taarifa hiyo Dr. Peter Mfisi alielezea kwa kiasi chake juu ya mambo mbalimbali ambayo yanamsumbua Rais Kikwete katika kuelezea ni kitu gani kilimsababishia kupoteza huko nguvu ambapo "Baada ya mapumziko ya dakika 10 hivi, Mhe. Rais alirejea kwenye shughuli hiyo na kuendelea kushirikiana na waumini wa AICT hadi mwisho wa ratiba yake."

Alielezea kuwa mojawapo ya hali zisizo za kawaida kwa Rais Kikwete ni tatizo la kwenye damu ambapo Daktari huyo wa Rais alisema kuwa "Rais ana damu nyingi. Hivyo, tumekuwa tunamshauri kupunguza damu kwa kuchangia Benki ya Damu. Tunashukuru amekuwa anafanya hivyo karibu kila baada ya miezi sita. Damu nyingi inaweza kuwa na madhara mwilini lakini Mhe. Rais hajafikia kiwango cha kuwa ni tatizo la kiafya."

Kati ya kauli ambazo ilizua utata kwa wachunguzi wengi wa siasa za Tanzania ni kauli ya daktari huyo kwa niaba ya jopo la madaktari wenzake kuwa "Napenda kusema wazi watu wote wasikie na kwa ukweli kwamba mimi na daktari mwenzangu yaani Dr. Mohamed Janabi hali ya afya ya Rais silo jambo linalotutia shaka wala kutusumbua au kutunyima usingizi." Tukio hili la majuzi linazidi kuhoji kama madaktari wa Rais bado hawakosi usingizi au hawajali juu ya afya nzima ya Rais kama inavyopaswa.

Katika ripoti yao ndefu hata hivyo walidokeza kitu ambacho duru nyingi za kiinteligentsia zinadokeza kuwa ndiyo kiini cha matatizo ya kiafya ya Rais Kikwete ambayo yanachangia matatizo mengine vile vile. Dr. Mfisi alisema kuwa "Tatizo pekee ambalo limekuwa likimsumbua Mhe. Rais mara kwa mara ni maumivu ya shingo yanayotokana na kuumia zamani utotoni na wakati wa ujana. Kuumia huko ni kwa baadhi ya pingili za uti wa mgongo, sehemu ya shingo **(cervical spine),** kuathirika na kumsababishia maumivu. Mara nyingi matatizo ya namna hiyo huwapata wanamichezo na wanajeshi. Kutokana na shughuli wazifanyazo. Kuumia siyo jambo la kustaajabisha."

Taarifa hii ilithibitisha tetesi za watu wengi kuwa Rais Kikwete ana matatizo ya kuinama mbele kwa muda mrefu na hivyo huwa anaonekana anapenda kusimama wima na simwepesi kugeuza shingo upande upande. Kutokana na maumivu haya ya muda mrefu vyanzo vya kuaminika kabisa vinadokeza kuwa amekuwa akitumia madawa makali ya kupunguza maumifu kwa muda mrefu ambayo mojawapo ya athari zake ni kukosa usingizi na hivyo kulazimika tena kutumia dawa nyingine za kusaidia kupata usingizi. Inajulikana kwa watu wa karibu kuwa Rais Kikwete hapati usingizi wa kutosha aidha kutokana na maumivu hayo au kutokana na dawa anazotumia ambazo nyingine athari yake ni kusababisha utegemezi wa madawa.

Tukio hili la karibuni la Rais kuanguka Jangwani katika mazingira yale yale kama ya 2005 na 2009 kunalazimisha kuhoji kama madaktari wa Rais walitoa taarifa kamili na ya ukweli au walitoa taarifa ambayo ilichangiwa na mambo ya kisiasa au la. Hii inatokana na ukweli kuwa katika taarifa yao hawakutoa maelezo ya kile ambacho nacho Cheche imenyaka kuwa ni taarifa zinazodaiwa kuwa Rais Kikwete amewahi kushauriwa kufanyiwa upasuaji unaohusiana na hizo pingili za shingoni zenye kumsababishia maumivu makali **(Inaendelea Uk. 3)**

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

AFYA YA KIKWETE

katikati ya miaka ya 2000 (2005?) lakini alikataa (au kushauriwa akatae). Hii inadaiwa ni kutokana na ukweli kuwa uchaguzi mkuu ulikuwa unakuja na alitaka kuwa katika nafasi ya kugombea na uwezekano mkubwa ni kwamba anazidi kuvuta muda ili akishapata nafasi ya kuingia madarakani kwa ngwe ya pili ndiyo tatizo hilo lishughulikiwe.

Hata hivyo maswali mengi bado yamebakia kati ya wananchi hasa wakizingatia jinsi kampeni zilivyo ngumu na ndefu na kama Rais Kikwete hatopata tena hali ya kuanguka kwani ikitokea tena itabidi itafutwe sababu nyingine ya kuelezea kwani karibu sababu zote ambazo zimetolewa hadi hivi sasa hazitoshelezi kuelezea hali yenyewe. Hofu kubwa ni kwamba kama jambo baya litatokea wakati huu kutokana na afya ya Rais Kikwete basi Chama cha Mapinduzi kinaweza kujikuta kulazimika kufikiria kupendekeza jina la mgombea mwingine.



Hata hivyo, vyanzo vya kuaminika ndani ya CCM vimeihakikishia kuwa Chama cha Mapinduzi kinauwezo wa kukabiliana na jambo lolote na wananchi wasiwe na wasiwasi kwani afya ya mgombea huyu wa CCM inaangaliwa kwa ukaribu na kama kungekuwa na jambo lolote la kusababisha asigombee basi Chama kingekwisha fikia maamuzi hayo. "Hadi hivi sasa hali ya afya ya Rais siyo ya kushtusha sana kama vyombo vya vya habari vinataka kuonesha; yeye mwenyewe ameridhika kuendelea na kampeni na chama kimeridhika na hivyo hakuna sababu yoyote ya kuwajaza wananchi hofu" amesema kiongozi mmoja wa CCM ambaye yuko katika kampeni ya Rais kanda ya Ziwa kwa masharti ya kutotajwa jina lake kwani si msemaji rasmi wa Kampeni.

Kama vile kuanguka kwa Rais Kikwete Jukwaani halikuwa tukio la uchuro au mkosi wa kutosha msafara wa Rais Kikwete huko Muleba umehusishwa na ajali ya gari ambapo mtoto mmoja wa shule ya msingi alifariki. Jana Jumatano kampeni ya Rais Kikwete huko Ngara nayo iliingiwa na kiwingu baada ya chopa yake (helikopta) kushindwa kufanya safari ya kuhutubia kampeni na badala yake kampeni hiyo kulazimika kuahirishwa hadi baadaye leo. Yote haya yametokea ndani ya wiki moja ya kampeni na wadadisi wa mambo ya kisiasa, na wadodosaji wa mambo ya kampeni wanaangalia wiki zilizosalia zinaleta nini kutoka kampeni ya CCM. **(Picha na Facebook ya Kikwete)**

NGUVU YA HOJA: CUF NA CHADEMA VIPI?

Na. M. M. Mwanakijiji

Wakati macho ya wengi hasa upande wa siasa za bara yameelekea kwa mgongano kati ya Chadema na CCM bado Chama cha Wananchi CUF kimejionesha kuwa kina wapenzi na mashabiki wengi tu pande za Tanzania bara.

Hata hivyo, kitendo cha wao vile vile kuacha majimbo kadhaa ya wabunge wa CCM kupita bila kupingwa na wapinzani kinaashiria kuwa bado upinzani Tanzania haujajua jinsi ya kujipanga na kutafuta njia mbadala za kupambana na mikakati na mbinu za CCM.

Tukizingatia kuwa CUF ndicho chama kikuu cha upinzani Tanzania kwa wakati huu na chenye raslimali na mfumo mkubwa zaidi basi ni fedheha kwa chama hicho nacho kama ilivyo Chadema kuweza kuangalia pembeni huku wabunge (wengine wakiwa wamegubikwa na kashfa) wakipita kama bibi harusi anayesindikizwa harusini.

Katika hili itakuwa ni upuuzi wa hali ya juu kulalamikia CCM au kudai kuwa CCM imewahujumu wapinzani. Kushindwa kusimamisha wagombea au kuhakikisha kuwa wagombea wanafuata taratibu zote zinazotakiwa ikiwemo kufanya mchujo mapema ni majukumu ya vyama vyenyewe na CCM.

Inashangaza kuona kuwa hata wao wapinzani wameshindwa kuweka mapingamizi ya kiakili kwenye majimbo kadhaa ya CCM au pale walipofanya hivyo imekuwa ni jukumu la wagombea mmoja mmoja bila kuuonesha umoja wa kichama.

Vyovyote vile ilivyo, CUF kama Chadema vimeonesha kuwa havikujipanga vizuri kuishtukiza CCM na badala yake wamejikutwa wakipigwa na mshangao huku CCM wakiendelea kupeta! Kuna matumaini?

DURU LA KIJASUSI - Na. Kanali "Xavier"

Kupita kwa baadhi ya wagombea wa CCM kwenye majimbo kadhaa kumezua maswali jinsi upinzani nchini ulijiandaa kwa uchaguzi katika majimbo hayo.

Maswali mengi katika duru la kijasusi wiki hii yanahusiana na kupita kwa wagombea huko Nyamagana ambapo Bw. Lawrence Masha aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika ngwe ya kwanza amepita katika kile kinachoonekana ni mizengwe.

Kupitata kwa Bw. Masha hata hivyo kunatarajiwa kutenguliwa baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kupatiwa ushahidi unaoonesha kuwa mizengwe na mbinu chafu vikiwemo vitisho kutumika dhidi ya mgombea wa Chadema jimboni humo na hivyo kumfanya Bw. Masha arudi kulitetea jimbo lake.

Hata hivyo, wagombea wengine ambao wamepita bila kupingwa hasa Mawaziri wameonesha tu udhaifu uliokuwepo katika maandalizi ya kampeni za vyama vya upinzani hasa katika kusimamisha watu ambao wanakubalika na waliofanyiwa utafiti ili kutotoa mwanza kama huu.

Udhaifu huu hata hivyo umedokezwa katika duru lililopita ambapo kitendo cha viongozi wa juu wa CHADEMA na CUF kugombea nafasi mbalimbali kumesababisha kupwaya kufuatilia na kusimamia zoezi la kutambua wagombea wanaokubalika na wenye uwezo wa kushinda.

Mwanakijiji, anaandaa barua ya wazi kwa Tume ya Uchaguzi kuhusu hili baadaye leo. Usikose!

Soma bure

DR. SLAA- "TUKUTANE JANGWANI"(toka Uk. 1)

Kwa mujibu wa Timu ya Kampeni ya Urais ya Dr. Kikwete ambao wanasimamia maandalizi ya mkutano huo mkubwa, Dr. Slaa atatoa hotuba ambayo itaonesha tofauti ya maono ya kiuongozi kwa taifa akitofautisha maono hayo na yale ya wagombea wengine wa Urais akiwemo Rais wa sasa Bw. Jakaya Kikwete.

"Dr. Slaa ataonesha ni kwanini Tanzania haiwezi kuvumilia tena miaka mitano ya watawala wa walioshindwa, sera mbovu na uongozi usio na maono yenye mwamko mpya wa ujenzi wa taifa" amesema mmoja wa wajumbe wa timu hiyo ya kampeni.


Naye Dr. Kitila Mkumbo ambaye ni miongoni mwa timu iliyosimamia uandikaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chadema amesema kuwa Tanzania haiwezi kupiga hatua ya haraka ya maendeleo bila uongozi wenye maono ya mabadiliko makubwa ya mfumo wa utendaji na utawala ambao utazingatia uwazi, kuwajibika, utawala wa sheria na usimamizi mzuri wa uchumi.

"Chadema itawapa wapiga kura uchaguzi wa wazi kabisa; wa kuchagua ubovu waliouzoea au mabadiliko ya mfumo bora, kuchagua sera zile zile goigoi au sera mpya na za msingi, viongozi wale wale walioonesha kushindwa au viongozi wapya ambao wanauwezo wa kulionogoza taifa" amesema Dr. Kitila.

Wakati huo huo, kampeni ya Dr. Slaa kuelekea Ikulu imeunda kikundi cha "Marafiki wa Dr. Slaa" ambao ni mjumuisho wa watu mbalimbali ambao ni washabiki wa kubwa wa kaza za Dr Slaa na walio tayari kutumia uwezo, mali, ujuzi na nguvu zao kumsaidia Dr. Slaa kwenda Ikulu.

Akinukuliwa na gazeti la Tanzania Daima mmoja wa wanamtandao huo wa marafiki wa Dr. Slaa Bw. Selemeni Rehani amesema kuwa "Marafiki wa Dk. Slaa (FOD) ni jumuiya kubwa ambayo inaundwa na watu mbalimbali wenye itikadi tofauti za vyama. Kundi hilo linaunganishwa na masuala ya msingi yanayolihusu taifa na linakerwa na ufisadi na umaskini wa Watanzania. Limeamua kuuanzisha umoja huo kuhakikisha mpiganaji wao anaingia Ikulu, kuleta maendeleo"

Kundi hilo limekutana jana Alhamisi



Bango la kampeni ya Dr. Slaa

ambapo maazimio mbalimbali yalichukuliwa. Hata hivyo, haijajulikana ni kwa kiasi gani kikundi hicho kitasaidia kumpatia Dr. Slaa Ushindi.

Na Da'Jessy: KUTURUSHA MOYO KWA NINI?



Sijui kama ni mimi tu au na wengine pia walijikuta roho zao zinashtuka walipomuona Rais Kikwete akianguka siku ya Jumamosi mbele ya kadamnasi ya wanaCCM na watazamaji wa luninga.

Najua wengi wameangalia suala hili katika mwanga wa kisiasa na kampeni lakini kwa upande wangu nimeangalia kama mama, mke, na binti na kuona kuwa kama ningekuwa na uwezo wa aina fulani ningemshawishi Rais Kikwete kujiengua na kampeni ili aende kushughulikia tatizo hili kuliko kuiweka familia yake na taifa roho juu kila anapojikwaa.

Inawezekana ni kweli bado anautaka Urais na anataka na yeye atimize miaka yake kumi kwenye kiti hicho cha juu kabisa. Lakini je inastahili kumuweka mkewe, watoto na taifa roho juu hasa kama tatizo lake ni kubwa zaidi ya "saumu"?

Sijui mama Salma na kina Ridhiwani wanachukuliaje kwani kwamba walikuwa wanalia na kushtuka tena inanifanya nielewe kuwa hawajazoea na roho zao zinakuwa juu juu wakati wote.

Kama hili ni kweli, ningeomba sana Rais Kikwete afikirie hekima ya kuendelea kugombea au kuendelea na madaraka hayo makubwa wakati afya yake bado ina matatizo makubwa. Mwisho wa siku hata hivyo ni familia yake ndiyo inapaswa kuwa na kauli ya mwisho kuhusu ugombea wake na yeye mwenyewe.

Niandikie: dajessy@klhnews.com

Soma Bure
hoja zenye nguvu

~ HASIRA YA BABA– 2 ~

(**Sule na Zawadi walichelewa kupata watoto, mara wakapata watoto wawili wa kike Shukuru na Majaliwa. Muda ulipita wakapata na mtoto wa kiume wakamuita Sifa. Kuzaliwa kwa sifa kulitarajiwa kuleta furaha, lakini kinyume chake kulianza kuchochea hasira ya baba, Endele)**

Hasira ya baba ilizidi siku kwa siku, miezi na miezi na mara miaka minne ilipita. Maisha yao pale nyumbani yakaanza kubadilika. Bila sababu ya msingi Sule alianza kuwa mkali sana kwa Sifa, kila alichofanya Sifa kwake ilikuwa kosa. Alipofanya kitu ambacho mwanzoni angemgombeza tu na kumkanya asirudie tena alichukua fimbo na kumtandika.

Mkewe alipomuuliza kwanini anamchapa sana mtoto Sule alimjibu ''anahitaji kufunzwa, kwani unalea yai hapa?''

Sifa nae alitengeneza woga kwa baba yake, alikuwa anaona yuko karibu na baba yake na alimpenda kweli lakini ukaribu huo waliokua nao mwanzoni ukaanza kupotea taratibu, baba yake alipokua nyumbani Sifa alinyong'onyea hivyo mara nyingi alikimbilia kucheza kwa jirani kitu ambacho kilimfanya asikose kuchapwa kila jioni kwa madai kwamba ''yeye ni mtoto wa kiume anatakiwa kulinda nyumba na sio kuzurura mtaani'' ila dada zake walipofanya hivyo hakukua na tatizo.

Kadiri hasira ya Sule ilivyozidi kukua makosa ya Sifa nayo yaliongezeka. Hata walipokua wakijumuika pamoja kupata chakula alitamani kumwambia hakaribishwi, kwanini ale chakula cha wanawe? iweje amlishe yeye, si aende kwa baba yake? Ila alijitahidi kujizuia. Mawazo hayo ya kutomtambua Sifa kama mwanae yalimzidia Sule na kuwa kama wingu kubwa lililotanga kwenye mawazo yake.

Mara kadhaa aliamua kumtolea uvivu kwakumsimanga kwa maneno ,''Mtoto unakula kama mchwa'' ''Hushibi uwaachie na wenzako'' tofauti na zamani ambapo alikua akiwasisitiza dada zake wamwachie yeye kwa sababu alikuwa ndiye mdogo, na wakati mwingine alimtaka Zawadi amuongezee ili aweze kukua kwasababu yeye ndie baba mwenye nyumba.

Ni kweli baada ya hasira ya mwanzo alijaribu kumpenda tena lakini jinsi maumbile ya Sifa yalivyozidi kuonekana kuwa hafanani kabisa na babake kwa nywele wala kwa kidevu, Sule uzalendo ukamshinda. Hata lile pendo la geresha alilojaribu likamtoka. Hasira yake ikamrudia tena kama kimbunga.

Zawadi alivumilia yote hayo akiwa na matumaini kwamba yatapita, ila siku zilivyozidi kusonga ndivyo Sule alivyozidisha visa dhidi ya mtoto. Alitamani dada zake nao wamchukie, hakufurahia kitendo cha wao kucheka, kucheza na kufurahi pamoja nae, alitamani wamtenge. Katika harakati zakufanikisha hilo, kila alipopata fursa alificha au hata kuharibu vitu vyao vyakuchezea ili lawama ziishie kwa Sifa. Jitihada zake hazikufua dafu, waligombana mara kadhaa ila hakuweza kupandikiza chuki kati yao.

Walimpenda mdogo wao na kila akichapwa na wao walijikuta wanalia na kumuombea msamaha kwa baba yao huku wakimlilia mama yao. Moyo wa majonzi ulianza kumzidia Zawadi vile vile; na machozi yaliambatana na majonzi hayo.

.

Siku moja Zawadi aliamua kumuuliza mumewe kama kuna tatizo lolote. Iweje awe mkali namna hiyo kwa mtoto? Alimwambia hata kama hataki kukubali ukweli ni kuwa yeye ndiye baba yake Sifa na inamuumiza kuona anamtenda vile mtoto wa nyonga yake. Zawadi alishangazwa kuwa mbona baadaye aliweza kubadilika na kuanza kumpenda lakini amebadilika na kuonesha chuki na husuda ya wazi kwa mtoto mdogo hivyo.

Sule alikuwa na jibu kila wakati, wakati mwingine alisema ''mtoto ameanza kukua, huu ndio muda wakumfanya mwanaume na sio kumkumbatia na kumdekeza kama unavyofanya wewe.''

Siku moja Sule aliamua kwenda mbali zaidi na kuonesha kuwa kweli alimaanisha anachosema. ''Huyu mtoto anatakiwa awe mbali na wewe hivyo nadhani tumpeleke kwa bibi yake akakae huko kidogo''. Zawadi alihamaki kwa maneno hayo ya mumewe. Alikumbuka kuwa hata maneno kuhusu Sifa yalipoanza pale kijijini Sule alishajaribu kutaka aondoke na mtoto aende kwa wazazi kwa muda naye alikataa kabisa. Alisema hana sababu ya kukimbia nyumba yake kwa sababu ya maneno ya watu.

Zawazi aling'aka ''Mume wangu,sasa watoto wakiondoka atabaki nani hapa nyumbani? Si tutakua wapweke sana?''

''We mwanamke usichoelewa nini? Sinimesema anatakiwa akae mbali na wewe kidogo? Huu sio mjadala, nilichosema ndicho kitakachokua na kama hutaki nitampeleka mimi mwenyewe'' Sule alifoka akiwa ananuka harufu ya kinywaji lakini macho yake yakiwa yanawaka hasira.

''Hapana mtoto wangu mi haendi popote''

(Itaendelea Wiki Ijayo)

TOA NAKALA 2 BURE

Kijarida hiki kitakuja kila wiki na habari motomoto na fikra kali za mabadiliko. Mawazo ya pande zote mbili yanakaribishwa kutoka kwa vyama na wagombea. Yasizidi ukurasa mmoja na yatatolewa kwa ridhaa ya Mhariri.

Tutumie: **mhariri@klhnews.com**

MHARIRI: MSAJILI NA TUME WAFANYE HAKI

Malalamiko ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo kuhusu upatikanaji wa fomu za Gharama za Uchaguzi kwa wagombea wake ni dalili tu ya tatizo kubwa ambalo linaonekana kwa makusudi au kwa bahati mbaya linadalili ya kupendelea chama tawala.

Kuanzia utaratibu wa kujaza fomu za wagombea na namna mapingamizi yamewekwa kwenye majimbo ni lazima ionekane kuwa haki inatendeka kwa vyama vyote isije kuwa kwa sababu hiyo hiyo mgombea mmoja anaruhusiwa kuendelea kwenye jimbo moja lakini kwa sababu hiyo hiyo kwenye jimbo jingine mgombea anaenguliwa.

NI lazima Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Tume ya Uchaguzi wahakikishe kuwa haki inatendeka na inaonekana kutendeka kwa vyama vyote bila kuachilia matatizo yasiyo ya lazima kutengeneza mazingira ya kuonekana wanabeba chama tawala.


Kwa vile tumekubali kujenga demokrasia basi ni lazima watawala wetu waoneshe kuwa wako tayari kulipa gharama yake ambayo mojawapo ni uwezekano wa chama kilichoko madarakani kuweza kuondolewa kwenye sanduku la kura. Vinginevyo, kama demokrasia wanafikiri ni ngumu basi wajaribu utawala wa kiimla!

.


—Mhariri


KATUNI ZA WIKI

PICHA YA WIKI



Prof. Ibrahim Lipumba akionesha Ilani ya Uchaguzi ya CUF kwa mwaka 2010-2015 (Habari Leo)





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com
Na
Http://www.JamiiForums.com

Facebook: "mimi mwanakijiji"

KUTOKA KWENYE MITANDAO YETU

Kuitoa ccm madarakani itachukua miaka zaidi ya 100 kwani matajiri wote wapo ccm,vijana wasomi wote wanakimbilia ccm,karibu kila mtu maarufu hata watangazaji wote wanataka CCM **(Anon, Issamichuzi Blog)**

Hongera jk kwa miaka 5 iliyopita ya uongozi bora ,hongera kwa dodoma university!big up usisikilize longo longo za wachache hawaitakii mema bongo— **(Anon, Issamichuzi Blog)**

Nimegundua kwamba kama ni mtu makini na unataka kuishi kwa amani nchi hii, usijaribu kuingia kwenye siasa. Nikirejea Gazeti la mwanahalisi toleo la tarehe18/8/2010 (nimesahau namba) jinsi lilivyozungumzia habari za kuenguliwa kwa bwana mdogo Bashe kweli nimeshawishika kutoa kauli hiyo iliyotangulia. Jaribu kupeperusha fikra zako za ukombozi wa taifa lako kwa njia nyingine kama ipo. **(Tembele2, Mwanakijiji.Com)**

Ndugu yangu Mwanakijiji, Kama sikosei uliwahi kuhoji AFYA YA RAIS wetu! ila tunaendelea kupata majibu mepesi ambayo yanazidi kutupa wakati mgumu sana na kutuongezea maswali mengi yasiyo na majibu. Ni kweli likija tokea jambo baya wengi watalaumiwa wakiwemo Madaktari wa Rais, na watu wengine wote walio karibu na Mheshimiwa **(Igembe Nsabo, Mwanakijiji.Com)**

Twajua kwa muda mrefu huwa hakipitii magazeti ya New Habari, lakini mengineyo yote huwa kinayapitia. Lakini leo (Augusti 22, 2010) asubuhi magazeti yote yaliyoandika habari za ukweli kuhusu tukio la jana la kudondoka jukwaani kwa Rais Kikwete hayakupitiwa na ITV . Magazeti yaliyopitiwa na kusomwa vichwa vyake vikuu vya habari vya mbele ni Nipashe, Habari Leo, Guardian, Sunday News, ambayo hayakuwa na habari ya tukio hilo kurasa za mbele.

ITV wanaficha nini? Kwa nini wanaficha ukweli? Mimi silalamikii sana kwa magazeti ya IPP kukosa kuandika habari za tukio hilo kurasa za mbele – lakini basi kituo hicho kingeruhusu watazamaji wapate habari za tukio kutoka kwenye magazeti ya wamiliki wengine. **(Marksman– JamiiForums.com)**

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: **http://www.mwanakijiji.com**

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*